



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA



Kumb. Na. KTV/MMC/A.40/2/61

27/12/2023

**Wananchi Wote,
TANZANIA.**

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI ZA AJIRA YA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda anawatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi ya kazi, katika kada ya Udereva. Nafasi husika ni kama ifuatavyo:-

1.0. DEREVA DARAJA LA II - NAFASI 3

1. SIFA ZA MWOMBADI

- i. Awe na Cheti cha kidato cha nne (Form IV) na Leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji Magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali
- ii. Awe amehudhuria Mafunzo ya Ufundu Stadi VETA au chuo kingine kinachotambulika na Serikali
- iii. Waombaji wenye cheti cha Majaribio ya ufundu Daraja la II watafikiriwa kwanza

2. MAJUKUMU YAKE:-

- i. Kuendesha Magari na Malori
- ii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya Magari
- iii. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- iv. Kufanya usafi wa gari
- v. Kufanya ukaguzi wa magari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- vi. Kufanya kazi zingine kadri atakavyo elekezwa na msimamizi wake

3. NGAZI YA MSHAHARA

Maafikiano / Majadiliano kati ya Mwajiri na Mwajiriwa kwa kada husika

2.0. MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBADI

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
2. Mwombaji aambatanishe nakala ya vyeti Elimu ya Sekondari na taaluma vinavyohitajika kulingana na kada husika kama ilivyofafanuliwa katika tangazo hili
3. Kila mwombaji aambatanishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa
4. **Uwasilishaji wa Vyeti vya kugushi utapelekea kuchukuliwa hatua za kisheria**

5. Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi (CV) akionesha namba za simu na anuani ya kwake na za wadhamini watatu (3) wa uhakika
6. Mwombaji aambatanishe picha ndogo (Passport Size) mbili (2) kwenye barua ya maombi
7. Waombaji watakaokidhi vigezo wataitwa kwenye usaili na watakaoshindwa kuzingatia masharti ya Tangazo hili hawataitwa
8. Mwombaji aandike nje ya bahasha kazi/kada/ nafasi anayoomba
9. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 02/01/2024
10. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta hivyo yatakayowasilishwa kwa mkono hayatapokelewa
11. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa,
S.L.P 216,
MPANDA.

Imetolewa na:-


Sophia Juma Kumbuli
**MURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
MPANDA.**


**VIKURUGENZI WA MANISPAA
MANISPAA YA MPANDA
S.L.P. 216
MPANDA-KATAVI**